# Mwongozo wa Jamii ya Mbinu wa Mgao wa Mfuko wa Kimataifa (Global Fund) 2017 – 2019

eannaso

Regional Platform
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

KABLA HATUJAANZA...

"MBINU YA MGAO" MAANA YAKE NINI?

## MBINU YA MGAO

=

## MCHAKATO WA MFUKO WA KIMATAIFA (GLOBAL FUND) WA KUAMUA KIASI GANI CHA FEDHA ZITAKWENDA KATIKA NCHI MBALIMBALI PAMOJA NA MAGONJWA

## UTANGULIZI

Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa (Global Fund) kwajili ya mwaka 2017-2022: "Kuwekeza katika kumaliza Majanga" inaazimia kulenga nchi zilizokuwa na mzigo mkubwa wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), Kifua Kikuu na malaria na zilizokuwa na uwezo mdogo wa kulipia mipango hii. Inaazimia pia kulenga watu maalum walio katika hatari ya maambukizi ya magonjwa haya matatu.Mbinu ya mgao inalenga katika kuimarisha [] kwa kupeleka idadi kubwa ya fedha hizi kwa watu hawa na sehemu zao.

Kufanya hivi, Mfuko wa Kimataifa inatilia mkazo nchi, maeneo na mikakat mingine maalum. Ina sera maalum ambayo inaongoza maamuzi ya jinsi fedha zitagawanywa miongoni mwa nchi pamoja na magonjwa.

- **MGAO UNAGAWANYWA KATIKA VIPENGELE VIWILI VIKUU**

### MGAO WA NCHI

Hii ni fedha inayogawiwa katika miradi katika ngazi ya nchi. Nchi zinaweza kupata bahasha zilizo na mgao wao wa mpango wa fedha wa mwaka 2017-2019 mwishoni mwa mwaka 2016.



### VICHOCHEO VYA UWEKEZAJI

Hadi kiasi cha dola milioni 800 zitatengwa kwajili ya Vichocheo vya Uwekezaji. Hizi ni fedha ambazo ziko nje ya mgao wa nchi na zitakuwa za vitu vitatu:

- Kuongeza motisha ya mgao wan chi kwajili ya mikakati maalum, kama vile kulenga watu maalum na walio hatarini, mipango ya kijinsia na mipango endelevu ya afya (zamani ikiitwa fedha za motisha)
- Mbinu za mgao mmoja kwa nchi nyingi ambapo mgao mmoja unasaidia zaidi ya nchi moja, ikiwa ni kwajili ya kurahisisha msaada ama kushughulikia masuala ya magonjwa katika mataifa mbali mbali (zamani ikiitwa msaada wa mataifa mbali mbali na kanda mbali mbali)
- Mipango maalum, kama vile fedha za dharura, mikakati ya kijamii, haki na jinisa, kuimarisha watu maalum pamoja na nyingine (zamani ikitwa Mkakati Maalum)

## JE KUNA KITU KIPYA KATIKA MBINU YA MGAO KWAJILI YA 2017-2019?

Kuna mabadiliko manne makubwa katika mbinu ya mgao wa mwaka 2017-2019 ukilinganisha na sera ya hapo awali ya 2014-2016:

- Hakutakua tena na “Majumuisho” ya nchi (ama kuwekwa pamoja kwa nchi kwa namna yoyote ile).
- Hamna fedha maalum iliyowekwa kwajili ya mgao wa motisha ama kwajili ya maombi ya fedha kwajilli ya kikanda (hata hivyo kutakua na fedha kwajili ya mipango hii miwili kama mpango mpya wa msaada wa ‘vichocheo vya uwekezaji”).
- Kutakuwa na mchakato mrahisi wa kuaamua marekebisho ya mgao wan chi kulingana na vipengele vya ufasaha na kuamua viwango vya chini vya msaada kwa nchi.
- Mfumo rahisi utatumika kuweka mapendekezo katika orodha ya Mahitaji Muhimu ambayo hayajafadhiliwa (Unfunded Quality Demand) (vitu ambavyo Mfuko wa Kimataifa wanadhani vinahitaji kufadhiliwa, ila hawana fedha za kutosha kwa muda huo).

## NI JINSI GANI MFUKO WA KIMATAIFA UTAAMUA KIASI CHA FEDHA KILA NCHI ITAPATA?

*Mfuko wa Kimataifa unaamua hii kupitia Mfumo wa Mgao. Mfumo huu unazingatia vitu vifutavyo:*

1. Mzigo wa maradhi (magonjwa) wa nchi
2. Uwezo wan chi wa kulipa (kiwango cha mapato ya nchi)
3. Viwango vya juu na chini vya gao (kiasi cha juu na chini cha fedha ambazo kila nchi inaweza kupokea)
4. Marekebisho ya nje kulingana na vigezo nje ya mfumo (sababu za ubora ambazo mbinu itakosa kuona, kama vile uwezo wa mfumo wa kimatibabu wa nchi ama sababu zingine za kimuktadha ambazo zitaadhiri mgao wa nchi)

## JINSI FEDHA ZITAGAWANYA MIONGONI MWA MAGONJWA HAYA MATATU

Hii inaitwa *“Mgawanyiko wa magonjwa”*

Japo waombaji wana urahisi wa kuamua jinsi ya kugawa fedha miongoni mwa mipango binafsi, kabla ya Sekretariati haijatangaza viwango vilivyopo katika bahasha za nchi itaamua (kwa makisio) jinis fedha zitagawanywa kati ya magonjwa matatu. Uwiano wa fedha za Mfuko wa Kimataifa wa mgao wa kipindi cha 2017-2019 utaganwanywa kama ifuatavyo:





## MABADILIKO MUHIMU KATIKA MGAO WA FEDHA AMBAYO NI MUHIMU KWA SISI KUFAHAMU!

10%

Kutakua na ongozeko la asilimia 10% kwa nchi za Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara 2017-2019

Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa sasa zitapokea asilimia 21.2% ya jumla ya rasilimali za Mfuko wa KImataifa. Katika mgao wa mwisho (2014-2016) nchi za Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara zilipata asilimia 16% za fedha zote.

Ongozeko la mgao mzima kwa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara inasukumwa na mgao mkubwa wa nchi za Kusini . Mgao wa nchi za Afrika MAshariki utaongozeka kwa asilimia 1% tu.

Kutakuwa na ongozeko la asimila 30% ya msaada kwa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zina idadi kubwa ya maambukizi ya Ukimwi katika wanawake na wasichana

25%

Kutakua na ongozeko la asilimia 25% katika nchi za juu 28 zilizokua na mzigo mkubwa wa 'multi-drug resistant TB (MDR-TB)

100 100

Kutakua na ongozeko la asilimia 10% kwa nchi zilizo na mzigo mkubwa wa malaria

%

Kutakua na ongozeko la asilimia 10% kwa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kwajili ya malariaa

Maeneo ya Ulaya ya Mashariki na Asia Kati zitatoka kupokea asilimia 4.7% hadi asilimia 2.4% ya jumla la mgao wa Mfuko wa Kimataifa. Hii ni punguzo ya kama nusu hivi.

Japo mataifa ya Afrika yatapata gao kubwa la 2017-2019 maeneo mengine yatapata kidogo. Eneo la Amerika Kusini na Caribbean mgao wake utashuka kutoka asilimia 3.5% ya jumla ya matumizi hadi asilimia 2% (punguzo la asilimia 43%).

## WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso